



TAARIFA KWA UMMA

(Imetolewa chini ya Kifungu na 19(2) (a) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414)

TAARIFA inatolewa kwa umma kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi ya leseni kutoka kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Rombo (Rombo WSSA) (“Muombaji”) kwa ajili ya kutoa huduma za majisafi na usafi wa mazingira katika Wilaya ya Rombo, Mkoa wa Kilimanjaro. EWURA inakaribisha maoni kutoka kwa wananchi juu ya maombi hayo. Maelezo ya Muombaji ni kama yalivyotolewa hapa chini:-

1: Jina na Anuani:

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Rombo,
S.L.P 244,
Rombo Mkuu.
Tanzania.
Barua Pepe: rombowssa@gmail.com

2: Maelezo ya Leseni:

Leseni ya kutoa huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika mji wa Rombo

3: Chanzo cha Maji na Miundombinu

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Rombo ina vyanzo vikuu vya maji vya aina mbili ambavyo ni maji ya juu ya ardhi na chini ya ardhi. Vyanzo vya juu ya ardhi vinajumuisha vyanzo 30 vya mto na chemchem na vyanzo vya chini ya ardhi vinajumuisha visima virefu sita (6). Jumla ya uwezo wa kuzalisha maji kwa vyanzo vyote ni mita za ujazo 26,825 kwa siku. Miundombinu ya uzalishaji na uhifadhi maji ya muombaji inajumuisha; matenki ya maji 112 yenye uwezo wa kuhifadhi maji kiasi cha mita za ujazo 11,999.5. Muombaji pia ana mtandao wa majisafi wenye urefu wa kilomita 1,374.85, pamoja na vilula mia sita themanini na mbili (682).

4: Umiliki

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Rombo inamilikiwa kwa asilimia 100 na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi kuhusiana dhidi ya maombi tajwa hapo juu, awasilishe kwa maandishi EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku 21 kuanzia siku ya kuchapishwa kwa tangazo hili. Nyaraka za maombi ya leseni zinaweza kuoneshwa kwa mtu yeyote kwa maombi maalum ya maandishi.

Mkurugenzi Mkuu

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
Jengo la EWURA, Kiwanja Na 3, Kitalu AD, Medeli Magharibi
S. L. P 2857, Dodoma.

Simu: +255-26 2329003-3; Nukushi: +255-26 2329005;

Namba ya Bure 0800110030;

Barua pepe: info@ewura.go.tz

Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>